REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Tuesday, 5th August, 2025

The House met at the Assembly Chambers at 2.30 p.m.

[The Deputy Speaker (Hon. Anthony Theuri) in the Chair]

PRAYERS

NOTICE OF MOTION

RENOVATION OF COUNTY ABATTOIRS

Hon. Anthony Theuri through Hon. Samuel Mugambi: Hon. Speaker, I beg to give notice of the following motion on behalf of Hon. Anthony Theuri;

THAT, AWARE THAT Agriculture including County abattoirs is a function of County Government as stipulated in part 2 of the fourth schedule of the Kenyan Constitution 2010;

FURTHER AWARE that Article 43 of the Constitution of Kenya guarantees every person the right to the highest attainable standard of health, including access to clean and safe food;

CONCERNED THAT the meat industry is a key contributor to food security and economic development in our County, and that safe and hygienic meat processing is essential for public health; COGNIZANT THAT the many existing slaughter facilities within the County operate under substandard conditions, with poor sanitation, lack of proper infrastructure, and inadequate waste management systems;

NOTING THAT the establishment of a modern and well-equipped slaughterhouse will promote hygienic handling of meat, reduce the spread of zoonotic diseases, improve infrastructure, create permanent job opportunities, and attract investment in the livestock value chain;

FURTHER NOTING THAT the lack of a centralized and modern slaughterhouse exposes residents to health hazards and denies local farmers and butchers a decent facility to process their livestock;

This House URGES the County Government to:

1. Carry out repairs and modernize the existing slaughter houses within the county;
2. Ensure the facility meets national and international hygiene and safety standards;
3. Incorporate modern technology and infrastructure in the design and operations of the slaughterhouse;
4. Employ permanent staff, including veterinary officers, meat inspectors, and skilled workers, to ensure proper operations;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

5. Engage stakeholders including local livestock farmers, traders, and the public in the planning and operation of the said facilities.

MOTION

RENOVATION OF COUNTY ABATTOIRS

Hon. Anthony Theuri through Hon. Samuel Mugambi: Hon. Speaker, I beg to move the following motion on behalf of Hon. Anthony Theuri;

THAT, AWARE THAT Agriculture including County abattoirs is a function of County Government as stipulated in part 2 of the fourth schedule of the Kenyan Constitution 2010;

FURTHER AWARE that Article 43 of the Constitution of Kenya guarantees every person the right to the highest attainable standard of health, including access to clean and safe food;

CONCERNED THAT the meat industry is a key contributor to food security and economic development in our County, and that safe and hygienic meat processing is essential for public health; COGNIZANT THAT the many existing slaughter facilities within the County operate under substandard conditions, with poor sanitation, lack of proper infrastructure, and inadequate waste management systems;

NOTING THAT the establishment of a modern and well-equipped slaughterhouse will promote hygienic handling of meat, reduce the spread of zoonotic diseases, improve infrastructure, create permanent job opportunities, and attract investment in the livestock value chain;

FURTHER NOTING THAT the lack of a centralized and modern slaughterhouse exposes residents to health hazards and denies local farmers and butchers a decent facility to process their livestock;

This House URGES the County Government to:

1. Carry out repairs and modernize the existing slaughter houses within the county;
2. Ensure the facility meets national and international hygiene and safety standards;
3. Incorporate modern technology and infrastructure in the design and operations of the slaughterhouse;
4. Employ permanent staff, including veterinary officers, meat inspectors, and skilled workers, to ensure proper operations;
5. Engage stakeholders including local livestock farmers, traders, and the public in the planning and operation of the said facilities.

Hon. Speaker, I am presenting this motion on behalf of Honourable Anthony Theuri, a Member representing Nanyuki Ward. I must say that this is a very legit motion of this time. When you are talking about improvement of the county, because you know very well, that this Laikipia County, 70 or 80 of us percent we farming, which is crop and animal.

In parts of Laikipia North, better part of Laikipia West, and even better part of Laikipia East, most people are farmers. They do livestock farming. I once said in this assembly that we have Rumuruti Livestock Market. I know people from Laikipia West, led by our senior former

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Deputy Mayor, long-time serving member of Igwamiti, Hon. Wachuka can attest to me that Rumuruti Livestock Market can be one of the leading livestock markets in East and Central Africa if we, as the county government and also in collaboration of the national government, put the appropriate measures.

Hon. Speaker, the reason why I am mentioning Rumuruti in regards to this motion, when you are talking about county abattoirs, and I know Hon. Gitahi is the chairperson of Agriculture Committee, he can attest to me that we cannot talk about livestock farming in Laikipia without improved and modern county abattoirs. I want to also give a statement here, but it might not be a very correct one, that one of the leading points where we collect a lot of revenue, and Hon. Lekopien can help us in this. It is Rumuruti Livestock Market, where we collect a lot of revenue every Thursday. But now the question is this one. We get a lot of returns, but we don't put investments in Rumuruti Market.

Honourable Speaker, if you go to most of these private ranchers, they have some modern abattoirs whereby a cow can take like 20 or 30 minutes to be slaughtered. But if you go to our own abattoirs, including the ones in Nyahururu, Gwa-Kung'u, Rumuruti, and Kinamba, I think a cow can take up to one hour or two hours. So now, the reason why Hon. Anthony brought this motion at this particular time, is that we as a county to improve our abattoirs and also put up some modern county abattoirs because we have the existing technology.

I have visited Kakuzi near Muranga Teachers College where we have a modern abattoir. If you have 100 cows and you want them slaughtered, they take less than two hours because they have chambers for every cow. If it is removing the skin, all the 100 cows will be removed skin at the same time. If it is cutting the stakes, it will happen simultaneously. As a County Government, this is something we need.

In the next Financial Year as we are planning our budget, Hon. Gitahi because you are the Chairperson for Agriculture, we need to put up a budget and set a modern abattoir. If you attend a livestock market on Thursdays in Rumuruti, there are a lot of lorries transporting live animals from Rumuruti to Nairobi. It could be cheaper to transport meat. So, they buy the cows and then they are slaughtered.

Hon. Speaker, this is a timely motion. Let us not just debate it here. Let us try and put up some measures that can be implemented. I am thankful that the National Government is putting up CAIP who are telling us that they will be putting up some abattoirs but we are not sure. As a County Government because Agriculture is a devolved function, we should put up our own modern abattoir, one in Rumuruti and the other one in Laikipia North.

You will find some private ranchers have their own private abattoirs. They slaughter and airlift meat to Nairobi and other places. Hon. Members who are here, that is one of the sectors that can bring economic growth to our county. Hon. Speaker, I want to stop there and when we talk about abattoirs, it is about livestock and people from Laikipia North are the experts who practise livestock farming and others. I want to request Hon. Lekopien to second the motion.

Hon. Parleto Lekopien: Thank you, Hon. Speaker. I stand in support of the motion. I also want to inform the Honourable Member for Salama that Salama is one of the biggest wards that rears a lot of animals. At some point, we are looking at Laikipia North but I think he should look at his home area because there are a lot of animals. Hon. Speaker, I stand and support the motion.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

This is a timely motion. We have had a few questions regarding the abattoirs in our county. As the Hon. Member has said, every Thursday we collect revenue of about Kshs 320,000 on cess fee including slaughterhouses and others. Hon. Speaker, as we support the motion, I urge Hon. Members and the County Government of Laikipia to support the abattoirs because as we continue, I saw one in Narok. They have a proper modern slaughterhouse. They even turn hides to proper shoes in the same place.

Hon. Speaker, I congratulate the mover of the motion. This is timely and we should invest in other different areas apart from it. As we slaughter the animals, we have the skins and hides. We can also do a tannery and we can process the skin and hides which can be sold locally and internationally. Hon. Speaker, I support the motion. Thank you.

(Question proposed)

Deputy Speaker: Hon. Members, the floor is open for debate. I will give this opportunity to Hon. Joseph Gitahi Macharia.

Hon. Joseph Gitahi: Asante, Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi ya kuchangia huu mjadala. Kwanza ninashukuru Mheshimiwa Mugambi kwa kusoma mjadala kwa niaba ya Mheshimiwa Anthony Theuri Mwakilishi wa Wadi ya Nanyuki. Kwanza, niko na changamoto kutaja hili jana ambalo Mheshimiwa Mugambi amesema ndiposa nikachukua lugha ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwape mfano kwamba tunahitaji vichinjio ambazo ni za kisasa. Kwetu Githiga, tuko na kichinjio ambacho ni cha kisasa. Sasa tunatarajia kifungue soko kutoka maeneo ya Kamwenje mahali ambapo mmesikia sana kuelekea maeneo ambayo inapakana na Mheshimiwa Karuiru kwenda katika kitovu cha siasa zetu za Githiga mahali ambapo panaitwa Kinamba.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwamba huu mswada kando na kutoa mapendekezo, kuna takwimu ambazo tunaona. Duniani kote tuna soko ya wafugaji ambayo iko na pesa sana. Saa hii ukipata mazungumzo na Mheshimiwa Rafiki yako kutoka Sosian, Mheshimiwa Lekopien Parleto, atakwambia kwamba kuna faida katika ufugaji.

Kuna faida katika Idara ya Mifugo. Wengi wametengeneza pesa kupitia hiyo biashara. Tunataka kuwaridhisha watu wa Laikipia hizo biashara ili wawe na pesa mfukoni. Unakumbuka tukiwa nawe, Mheshimiwa Spika, tuliwaambia watu wa Laikipia kwamba tunataka pesa mfukoni. Sisi tunataka tuwe na vichinjio vya kutosha ili tuwe sawa na wengine duniani kote. Vichinjio vya kisasa vinaweza kukagua na kubaini magonjwa kwenye nyama ambayo yanatuzuia kuuza bidhaa zetu kwenye soko za kigeni.

Kwa hivyo, Mheshimiwa Spika, nataka kuukaribisha huu mswada na kuunga mkono sana kwa sababu, kwanza kabisa, tutapata nyama yasiyo na magonjwa. Pili, tunataka soko ya mifugo iweze kunoga. Wenye wamefuatilia masoko yetu, kuna barabara ambayo tumetengeneza kutoka huko Arabal, kuenda Muchungui, kupitia hapa Karandi na kuenda hadi Rumuruti. Inafika kwenye kivukio cha wanyama pori wanaoweza kuliwa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunataka kusema kwamba ni muhimu sana katika hii Kaunti yetu ambayo yasemekana ina mchanganyiko. Sitaki kuongea Kiingereza kwa sababu kuna Kanuni ya Bunge inayosema kwamba tusichanganye lugha. Hata hivyo, kuna sheria inayosema kwamba Laikipia yetu ni ya wanyama. Nikitohoa, ni kwamba Laikipia ni *cosmopolitan.* Hio inamaanisha kuwa tunao wafugaji, watu wanaofuga wanyama na wakulima. Ni muhimu sana tupate hizi soko ili tupate kitu cha pili pia, ambacho ni mfumo wa kisasa.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Mheshimiwa Spika, ukifanya utafiti utapata kwamba... kuna Mbunge anayeongea kwa sauti ya juu na kutatiza mtiririko wa mawazo yangu. Hata hivyo, nataka kusema kwamba hivi vichinjio ni muhimu sana. Bali na kupata nyama safi na uchuuzi wa kisasa, vichinjio vilevile vinatoa nafasi za ajira. Nataka kumpongeza Mheshimiwa Mugambi ambaye ameona ni vyema kuongea kuhusu hilo jambo; kwamba tukitengeneza vichinjio vya kisasa tutakuwa na ajira zaidi. Hio ni kwa sababu hatima ya sisi kuhakikisha kuwa tunatafuta pesa kupitia ufugaji ni hili jambo la soko. Ni muhimu sana tupate soko ambayo ni safi ili watu wengi kutoka nyanja tofauti tofauti waweze kuchangia katika soko letu la nyama.

Vilevile, Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba nimeangalia makadirio ya bajeti mwaka uliopita. Nina uhakika kuwa hawa wawakilishi wadi, hususan wanaotoka vijijini; wajua sisi sio watu wa mtaani. Kwa wale wanaotoka vijijini, tutahakikisha kuwa tunaongeza utajiri kwenye mifuko ya watu.

Nikimaliza, nataka kusema kwamba sio swala la vichinjio pekee. Kwenye hili gatuzi letu lazima tuhakikishe kuwa kuna dawa zinazotumiwa na mifugo. Nimemsikia Rais akipiga kampeni ya kutoa chanjo kutoka huko Kajiado hadi mahali pengine. Tusipopata hizi dawa ambazo ni muhimu, nyama yetu itakataliwa kwenye soko la kimataifa.

Kwa hivyo, nataka kusema naunga mkono huu mswada. Huu mswada vilevile umetoa mapendekezo. Kuna mambo ambayo wametaja na yanapaswa kufanywa na hili Bunge pamoja na gatuzi letu la Laikipia ili kuhakikisha kuwa nyama yetu inauzwa katika masoko yote. Nataka kuwasihi Wajumbe wote tulio nao siku ya leo waunge mkono huu mswada ili tuwe na nyama safi, tufanye biashara na ukulima. Asante sana.

Hon: Irene Wachuka: Asante sana, Bwana Spika. Nasimama mbele ya Bunge letu kuchangia mswada. Naanza kwa kumshukuru aliyeuleta mswada, Mheshimiwa Theuri, ambaye ndiye Mwakilishi wa Wadi ya Nanyuki. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Mugambi Gatati ambaye ameusoma mswada jinsi ambavyo umeandikwa. Nimemsikia Mheshimiwa kutoka Githiga vile ameongea. Tukisema ukweli, sisi tumelala kidogo na lazima tuamke.

Tuko na utajiri mwingi sana kwenye upande wa Laikipia Kaskazini na Laikipia Magharibi, ambapo pana soko kubwa sana pale Rumuruti. Ukienda pale siku ya Alhamisi, unaona malori kutoka pembe zote za nchi yanakuja kununua mifugo. Kama ambavyo mwenzangu amesema, ni vizuri tuwe na vichinjio vya kisasa kwa sababu faida itabaki kwetu. Ng'ombe wakichinjwa pale, ngozi inabaki hapo, na hiyo ni biashara nyingine. Akibeba nyama yake, kuna vitu ambavyo atawacha. Kwa hivyo, nataka kusema kwamba mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo katika hili Bunge atafute muda. Kama ningeulizwa, singesema wanachama wa Kamati ya Kilimo pekee waende.

Twende tutembee pahali nasikia Mheshimiwa Mugambi anasema tuone zile vichinjio imejengwa ya kisasa, ukikuja Nyahururu ikuwe na hiyo moja pia ukienda Rumuruti na kaskazini. Hata kaskazini iko na Ng'ombe mingi sana na mbuzi kila mahali Kaunti la Laikipia nzima, tuwe na vichinjio tatu au nne vya kisasa ambavyo vitakuwa vikitusaidia.

Wakati wa bajeti, naona pesa mingi ikiwekwa kwa Idara ya kilimo, serikali kuu inapeana pesa mingi kwa kilimo. Mimi ningeomba mwenyekiti wa kilimo aamuke tufanye kazi, tulete utajiri kwetu na tujue ile mambo ya zamani iliisha ili tuendelee na mtindo ule uko wa kisasa. Kwa hivyo, nasimama kuunga mkono na kusema asante sana na mungu ambariki.

Hon. Daniel Mugweru: Asante sana, Mheshimiwa Spika, naona mtindo ni huo huo wa kuongea lugha ya Kiswahili, kwa hivyo, mimi nimesimama kuunga huu msaada mkono ambao umeletwa na Mheshimiwa wa Salama; Gatati. Ni mzuri tuseme ukweli ya Kamba Mheshimiwa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Gitahi kama amesema msaada huu umenoga, ni kweli umenoga. Kwa hivyo hata mimi naomba tuwe na vichinjio. Hata Umande kuwe na kichinjio ukienda huko, Salama kuwe na kichinjio ili hata sisi tutasaidika na mambo mengine mengi huko tunaachiwa vitu na tuweze kuwa kama vile Mheshimiwa Gitahi amesema; sisi wote tuwe na nyama nzuri. Asante sana, naunga mkono.

Deputy Speaker: Honourable Members, before I put the question, I would like to thank one of our Honourable Member Hon. Gatati for articulating the motion on my behalf and I take this opportunity for the proposer to reply.

Hon. Samuel Mugambi: Nataka pia kushukuru Wabunge waliojadili hii mjadala, na ni mjadala muhimu sana Bwana Spika. Pia, nimeshika kabisa vile Mheshimiwa mama yetu, Mheshimiwa Wachuka amesema. Amenena jambo la maana sana, sijui kama nyinyi wengine mumelisikiza vizuri. Amesema kwamba hii hata haistahili kuongozwa na kamati ya kilimo, hii inastahili sisi wote tukuwe pale kipao mbele. Ningetaka kuambia Mheshimiwa Wachuka kwamba kuna vichinjio kubwa na mzuri sana za kisasa. Moja iko hapo Kakuzi na kuna zile ziko Nairobi na pia ile mahali nzuri sana.

Ningeomba Mheshimiwa Spika hawa Wabunge wapelekwe ile mahali nzuri sana tunaweza soma, nilienda hapo nikiwa na miaka ishirini na Afrika kusini mahali kunaitwa Crake. Hapo ndiyo kichinjio ile nzuri zaidi katika Afrika nzima sasa huko Afrika Kusini na kutoka hapa kama huu mwezi tunaenda Arusha, tubadilishiwe tupelekwe Afrika kusini, twende tusome hiyo na tuilete hapa kwetu Laikipia.

Ukiangalia Afrika Kusina kuhusu ukulima wa ng'ombe, pia hapa hayo maneno yameanza. Sasa hivi ukiangalia kama Mheshimiwa Lekopien, wameanza kubadilisha zile kondoo za awali na kuleta dorper ambayo ni nzuri sana. Unaweza kuta ikisaidia jamii yao sana kwa sababu unapata ya kwamba ile kondoo ya kienyeji ikiuzwa elfu kumi na tano lakini dorper inauzwa elfu mia moja.

Juzi Mheshimiwa Lempaira alichukua hiyo jukumu ya kwenda Afrika Kusini na pia Namibia maanake hizo ndizo zile nchi ambazo zimeongoza kwa ukulima wa ng'ombe, mbuzi na kuku. Alileta mbuzi zake hapa Kenya na huo ndio mwelekeo ambao tunafaa kupatia wakaazi wetu wa Laikipia.

Ndio maana naona huu mjadala wa mambo ya vichijio ukiwa mazuri sana. Nasikitika sana nikiona mahali kama Rumuruti magari zikifurika, zinachukua ng'ombe na kuzipeleka Nairobi na Kisumu. Naelewa vizuri ya kwamba kama hizo ng'ombe zingebebwa kama zimechinjwa, ingekuwa angalau lakini huyu mtu kubeba mzigo wa ng'ombe ishirini au mia, huo ni mzigo mkumbwa. Pia kuna hasara ambazo zinaweza kutokea barabarani. Unapobeba ng'ombe zikiwa uhai, zikifa ni kumaanisha hizo ng'ombe haziwezi kutakika.

Mheshimiwa Spika, pia mimi ningetaka kushukuru kwa sababu haya ni mafikira yako na umefikiria wa Laikipia vizuri. Kwa hivyo, ni vizuri hii mijadala tusiwe tu kazi yetu ni kuongea hapa. Sisi huwa tukisema kila wakati Serikali ya Laikipia, hii serikali ni kina nani? Serikali ya Laikipia ni sisi na kwa hivyo, ningeomba hili Bunge ya kwamba tukitoka likizo tuweze kubadilisha kidogo.

Hii mijadala ambayo tunaongelea hapa, kwa maoni yangu tungebadilisha. Tukileta mjadala muhimu kama huu, tukimaliza wiki mbili tunaita idara ambayo inahusika. Tunaita Waziri wa Shirika na Waziri wa Kilimo na tunaketi na hao chini tuweze kufuatilia mijadala muhimu kama hizi ili isiwe ya kwamba kazi yetu ni ya kuongea tu. Hata leo niliona ya kwamba kuna mtu ambaye alikuwa anatupiga picha hapa na ni vizuri kwa sababu hatufanyi kazi ya haramu.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Ni vizuri pia hata sisi watupatie heshima yetu kwa sababu hauwezi enda kwa boma ya mtu na kuanza kupiga picha bibi na watoto. Ni lazima uwe umepewa ruhusa. Ninashukuru na pia ni vizuri tufuatilie mijadala ingine muhimu kama huu. Nimesikia Mheshimiwa Gitahi amechangamka sana na kunoga kwa Kiswahili na ni vizuri. Hata sisi tunaambiwa leo hii tutakuwa tunajadili kwa Kiswahili. Ule mtu ambaye nimesikia akilemewa kabisa ni Mheshimiwa Mugweru. Huyo imebidi ameongea kwa dakika moja na kuketi haraka kwa sababu maneno mengine yanakuwa ngumu.

Kiswahili pia ni lugha ya taifa na hata ukienda mahali kwingine kama shule, utapata masomo ya Kiswahili ambapo watoto hujibu mtihani kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, ni vizuri hata sisi tunasimama kama mwelekeo kwao ya kwamba unasoma kwa Kiswahili na Kizungu. Sasa yule mtu ambaye amebakisha, tukileta huo mjadala mwingine ni lazima Mheshimiwa Karuiru aongee kwa Kiswahili ndio tusikie Kiswahili chake cha huko Ol Moran kimetoshana namna gani. Kwa hayo mengi na machache, asante sana.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Deputy Speaker: This House now stand adjourned until tomorrow Wednesday, 6th August, 2025 at 10.00 a.m.

The House rose at 3.24 p.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*